**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
***OFISI YA RAIS***
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA MKURANGA**

**Kumb. Na.LD/MK/9643/9** 1/3/2026

Mkurugenzi Mkuu
Mamlaka ya Uwekezaji na Maeneo Maalumu ya Kiuchumi Tanzania (TISEZA)
S.L.P 6775,
**Dar Es Salaam.**

**YAH: KIWANJA NA. 113 KITALU 'N' DUNDANI, WILAYA YA MKURANGA**

Rejea mada tajwa hapo juu,

2. Ninachukua fursa hii kuijulisha Ofisi yako kwamba, Kampuni ya **Suomei Investment and Development Limited** imenunua maeneo kutoka kwa wananchi mbalimbali na sasa upangaji na upimaji umekamilika nae neo hili linajulikana kama kiwanja Na.113 kitalu "N" Dundani kwa matumizi ya kiwanda cha huduma

3. Kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi **Na. 4 ya 1999, fungu la 19-20**, Tangazo la Serikali **Na.72 la tarehe 4/5/2001,** Kanuni za Ardhi za 2001, **kanuni ya 9C (v),** kiwanja hiki kinatakiwa kuwa miliki ya Mamlaka ya Uwekezaji na Maeneo Maalumu ya Kiuchumi Tanzania (TISEZA).

4. Halmashauri ya Wilaya inaitambulisha Kampuni hii kutoka nje ya nchi kwako ili iweze kupatiwa Certificate of Incentives kwa kuwa kiwanja hiki ni halali na hakina mgogoro wowote.

Naomba kuwasilisha kwa hatua zako muhimu.

HALMASHAURI YA WILAYA
K.n.y: MKURUGENZI MTENDAJI (W)
MKURANGA

Chagiye R.M
**K.n.y:** Mkurugenzi Mtendaji (W),
**Mkuranga.**

**Nakala:** Mkurugenzi Mtendaji (W),
**Mkuranga**-------Kwa taarifa

Suomei Investment and Development Limited
**Dar es salaam**--- kwa ufuatiliaji